# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA

**MUHEZA.**
**TANGAZO** **30/04/2018**

## TANGAZO LA ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI MAPATO MBALIMABALI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI 2018 HADI JUNE 2019 KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ZABUNI NA. LGA/132/HQ/2018/2019/NC/01

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza anawatangazia Wananchi / Wafanyabiashara/Makampuni/ushirika/vikundi kuwa anahitaji kupata mawakala wa ukusanyaji mapato katika maeneo mbalimbali ya Halmshauri ya Wilaya ya Muheza kama yalivyoainishwa hapo chini;

| S/N | MAELEZO | NAMBA YA ZABUNI |
|---|---|---|
| 1. | UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU WA MAZAO YA NAFAKA,MATUNDA,VIUNGO NA MENGINEYO ISPOKUWA MAZAO YA MISITU,KATANI,KOROSHO, MPIRA,CHAI NA MASAMBO | LGA/132/HQ/2017/2018/NC/01 |

**3. Masharti kwa Waombaji:-**

1. Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania
2. Mwombaji awe na uwezo wa kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa Kielekroniki (Electronic Revenue Collection System).
   i. Mfumo wa kielektroniki unaotumika na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ni Local Government Revenue Collection Informaction System – LGRCIS.
   ii. Wakala atatakiwa kuonyesha idadi ya **(Point of Sale- POS Machine)** atakazotumia, ikiwa ni pamoja na maeneo zitakapotumika (vituo vya kukusanya mapato). Muombaji atakaye fanikiwa kupata kazi atatakiwa kutumia mashine za kukusanyia mapato ambazo zimeunganishwa na mfumo wa mapato wa Halmashauri
   iii. Stakabadhi zitakazotumika kukusanya ushuru zitapatikana Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na zitakuwa ni za mfumo wa kietroniki
   iv. Mapato yote yatakayokusanywa na wakala yataingizwa katika Akaunti ya Halmashauri na wakala atalipwa kwa asilimia. Muda wa malipo kwa wakala ni ndani ya siku saba [7] ya mwezi unaofuata baada ya wakala kuleta hati ya madai husika.

v. Kila mwombaji anatakiwa kufanye utafiti kwenye eneo la mapato analotarajia kuomba na kuonyesha kiasi cha mapato atakachokusanya kwa kila baada ya miezi mitatu ndani ya mwaka mmoja.

vi. Wakala atawajibika kuwasilisha makusanyo katika akaunti ya Halmashauri kila wiki au kila baada ya siku saba (7).

vii. Wakala aonyeshe asilimia itakayolipwa baina yake na Halmashauri pamoja na mchanganuo wa mapato, matumizi na faida. Na ikumbukwe kwamba kuweka kiwango kidogo cha asilimia ya malipo sio kigezo pekee cha kupata zabuni, mchangunuo wa mapato na matumizi ndio utakao toa picha ya uhalisia wa kiwango cha asilimia ya muombaji.

viii. Muombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya wilaya muheza

ix. Ada ya maombi ya zabuni ni **Tshs. 100,000/=** zilipwe kwenye akaunti ya Halmashauri na kupewa stakabadhi pamoja na kabrasha la zabuni ambalo atatakiwa kulijaza na kulirudisha kabla ya muda wa mwisho kupokea maombi, Ada ya maombi hairudishwi.

x. Gharama za ukusanyaji ushuru ni juu ya wakala mwenyewe

xi. Muombaji awe na Leseni hai na inayofanana na Biashara husika

xii. Muombaji awe na usajili wa kuandikishwa kwa Kampuni/Ushirika/vikundi

xiii. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atayehusika na zabuni hii

xiv. Muombaji awe na uzoefu katika ukusanyaji wa mapato usiopungua miaka 3 (Ambatanishe na barua za uteuzi wa kazi hizo)

xv. Wakala atakayeshinda zabuni hii atawajibika kuweka Dhamana ya utendaji ya fedha taslimu, asilimia 10% ya fedha anazotarajia kukusanya kwa miezi ya mkataba na malipo hayo yatafanyika kabla ya kusaini mkataba. Wakala anapaswa kuweka fedha hizo ndani ya siku saba (7) za kalenda baada ya kupata barua ya kukubaliwa kupewa kazi. Na wakala atakayeshindwa kuweka fedha za dhamana ya utendaji kazi katika muda wa siku saba (7) atakuwa amejitoa katika zabuni hii, na atapewa muombaji mwingine.

xvi. Muombaji ataje eneo la Kampuni au biashara ilipo ( physical location )

**xvii.** Mkataba utakuwa wa miezi 12 kuanzia tarehe **01 Julai 2018 hadi tarehe 30 Juni 2019**

xviii. Viwango vya kutoza ushuru ni vile vinavyopitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kulingana na sheria ndogo

**xix.** Waombaji wa zabuni ya mazao ya nafaka, matunda, viungo na mengineyo isipokuwa mazao ya misitu, **hawaruhusiwi** kukusanya mazao ya **chai,mkonge,masambu,mkonge,korosho na mpira** kwani mazao hayo yanakusanywa na Halmashauri yenyewe

xx. Muombaji awasilishe mpango kazi wa kuonyesha jinsi atavyotekeleza kazi hiyo.

xxi. Asilimia 20% itatozwa kwa wakala atakaye chelewesha marejesho yake ndani ya siku 5 kulingana na tarehe ya marejesho ya mkataba.

xxii. Mwombaji aonyeshe uwezo wa kifedha wa kufanya kazi. Aambatanishe Bank ya kuanzia januari 2018 hadi siku ya kutoka kwa tangazo hili.

xiii. Maelekezo mengine ambayo mwombaji anapaswa kuzingatia yanapatika katika kablasha la zabuni.

xxiv. Maombi yafungwe katika bahasha kwa lakiri (Seal) na kuonyesha namba ya zabuni kwa kila zabuni anayoomba'

xxv. Muombaji aliyewahi kupewa kazi na Halmashauri ya Wilaya Muheza na Taasisi nyingine na akashindwa kutimiza masharti ya utendaji kazi ombi lake halitafikiriwa.

xxvi. Muombaji hatakiwi kuwa mtumishi au Kiongozi wa Halmashauri ya wilaya muheza.

xxvii. Zabuni zote zitakazochelewa kulingana na muda uliooneshwa katika Tangazo la zabuni hazitafunguliwa

xxviii. Kabrasha za zabuni zinapatika katika ofisi ya Afisa Manunuzi wa wilaya (PMU OFFICE) kuanzia saa 1.30 Asubuhi hadi 9.30 alasiri siku za kazi. Mwisho wa kupokea zabuni ni siku ya jumatatu tarehe **14/05/ 2018 Saa 4.30 asubuhi** na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi tu baada ya zabuni zote kupokelewa. Zabuni zitafunguliwa mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria.

**JINSI YA KURUDISHA ZABUNI**

Muombaji atatakiwa kujaza fomu husika na kutoa maelezo kwa ufasaha kulingana na maelezo yaliyopo katika kabrasha la Zabuni.

Kabrasha la Zabuni baada ya kujaza kama ilivyoelezwa hapo juu itolewe nakala moja, zote mbili kwa pamoja zifungwe kwenye bahasha na kuwekwa lakiri (seal). Juu ya bahasha iandikwe jina la zabuni na namba ya zabuni unayoomba, juu ya bahasha isionyeshwe alama ya aina yeyote mbali na tulivyoelekeza hapo juu na itumwe kwa:

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA**
**S.L.P. 20,**
**Muheza.**

*Limetolewa.*

Luiza O.Mlelwa
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA**